

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI**  
**(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**

Kumb. Na. MDC/E.50/3/VOL IV/67



22/03/2018

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi anawatangazia wataanzania wote wenye sifa kuomba kazi ya Mtendaji wa Kijiji III kwa masharti ya kudumu. Tangazo limetolewa baada ya kupokea kibali cha ajira mbadala chenye Kumb.Na.CFC 26/205/01 "FF"/91 cha tarehe 22 Agosti, 2017 pamoja na barua ya nyongeza ya muda wa utekelezaji wa kibali cha ajira mbadala ya Watendaji wa Vijiji na Mitaa chenye Kumb.Na.CFC 26/205/01 "GG"/95 cha tarehe 12/03/2018.

**1. Mtendaji wa Kijiji Daraja la III TGS B – Nafasi 23**

**Sifa ya Mwombaji.**

Elimu ya kidato cha nne/sita aliyehitimu mafunzo ya Astashahada katika moja ya fani ya **Utawala, Sheria, Maendeleo ya Jamii, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha na Sayansi ya Sanaa** kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**Kazi na Majukumu.**

- Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- Kusimamia na kutafsiri Sheria, Sera na Taratibu
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- Kusimamia, Kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi

- Kusimamia utungaji wa Sheria ndongo za Kijiji
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

Mshahara kwa mwezi utanza na **TGS B<sub>1</sub>** yaani **390,000/=** kwa mwezi

**Masharti ya jumla:**

1. Mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzani.
2. Awe na umri wa miaka 18 na usiozidi miaka 45.
3. Maombi ni lazima yaambatane na wasifu binafsi (CV).
4. Maombi nilazima yaambatane na vivuli vya vyeti vya kidato cha nne au sita.
5. Maombi nilazima yaambatane na vivuli vya vyeti na Taaluma.
6. Maombi ni lazima yaambatane na kivuli cha cheti cha Kuzaliwa .
7. Picha mbili (2) Passport size.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **04/04/2018** saa **9:30** Alasiri pia tangazo hili linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri [www.moshidc.go.tz](http://www.moshidc.go.tz) na kwenye mbao za matangazo, maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:

**Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P 3003,  
MOSHI.**

Tangazo limetolewa na :-

  
Amani.A.N

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA  
MOSHI**

*Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya Wilaya  
Moshi*